

Mielekeo ya Lugha na Ruwaza za Matumizi ya Lugha ya Walimu wa Kiswahili wa Shule za Msingi katika Kaunti ya Siaya

*Eric W. Wamalwa, Ernest S. Mohochi na Isaac Ipara Odeo
Chuo Kikuu cha Kibabii*

Ikisiri

Makala haya yalichunguza na kubainisha mielekeo ya walimu wa Kiswahili katika shule za msingi za kaunti ya Siaya. Aidha, ruwaza zao za matumizi ya lugha zilipambanuliwa. Data ilikusanywa kwa kutumia hojaji. Wasailiwa 34 waliteuliwa kutoka kaunti ndogo sita za kaunti ya Siaya. Data ilichanganuliwa kwa mkabala mseto kwa kutumia njia za kitakwimu na kimaelezo. Matokeo ya utafiti yamewasilishwa kupitia njia za maelezo na majedwali. Matokeo ya utafiti yameonesha kwamba walimu walikuwa na mielekeo kubalifu kuhusu Kiswahili. Aidha, ruwaza za matumizi yao ya lugha zilidhihirisha kwamba matumizi ya Kiswahili yamezidi kupanuka katika mawanda mengi ya kijamii katika Kaunti ya Siaya.

Maneno Muhimu: Mielekeo ya Lugha, Ruwaza za Matumizi, Kiswahili, Lugha na Jamii

Utangulizi

Mielekeo ni moja kati ya dhana za taaluma ya sayansi-tabia iliyoshughulikiwa na watafiti kwa zaidi ya karne moja iliyopita. Mielekeo imefanyiwa uchunguzi mwingi na matokeo yake kuchapishwa katika taaluma za saikolojia, isimujamii na saikolojia jamii ya lugha (Kircheri, 2010). Kwa kuwa tafiti hizo zilifanywa kwa misingi ya taaluma mbalimbali, hakuna fasili ya moja kwa moja ya mielekeo. Hata hivyo, fasili zifuatazo zitaufaidi uchunguzi huu.

Gardner (1985) amesema mielekeo inaelekezewa kitu au jambo fulani; na imani ya mtu kuhusu kitu au jambo fulani ndiyo msingi wa mielekeo yake. Watu basi wanatathmini matendo kabla ya kuyatenda wakiongozwa na mielekeo. Mtu anapoamini kwamba lugha fulani haifai, huenda akawa na mielekeo hasi kuihusu. Mielekeo hiyo inaweza ikaathiri matumizi yake ya lugha husika. Hali hiyo inatokana na ukadiriaji wa ubora au udhaifu pamoja na umuhimu wa kilengwa. Istoshe, ni tokeo la utambuzi kwamba jambo au kitu fulani ama kinaweza kuwa na manufaa au upungufu fulani. Maoni kama haya yameshikiliwa na Bohner (2001) anapoeleza kwamba kwa kiwango cha mtu binafsi, mielekeo huathiri mtizamo, fikra na tabia. Lakini kwa kiwango cha kikundi, mielekeo huathiri ushirikiano au kuchochea uhasama baina ya washiriki wa kundi moja na jingine.


Williams (1974) katika Fasold (1984) ameeleza kwamba mielekeo ni hali ya kiakili inayoibuliwa na kichocheo fulani kinachomfanya mtu atoe mwitikio hasi au chanya. Kwa hivyo, mielekeo haibainiki wazi kwani ni hali ya kiakili tu. Ni msimamo wa kiakili ambao uchunguzi wake hutegemea habari za watafitiwa kuhusu maoni yao juu ya kilengwa husika. Jambo linalosisitizwa katika ufafanuzi wa mielekeo ni hali ya kuwa tayari kiakili (Agheyisi na Fishman, 1970).

Zimbardo na Leippe (1991) wanasema mielekeo ni tathmini inayofanyiwa kilengwa fulani kutokana na utambuzi au ufahamu kukihusu, pamoja na kudhihirisha mwitikio wa kihisia na kivitendo kukihusu. Isitoshe, wameeleza kwamba mielekeo inaweza kuathiri ufahamu, hisia na nia ya tabia za mtu katika nyakati za baadaye. Maelezo haya yanaashiria sifa muhimu ya mielekeo. Mielekeo ina muundo. Muundo huo ni wa utatu. Ina sehemu tatu ambazo ni sehemu ya ufahamu/utambuzi, sehemu ya hisia na sehemu ya vitendo. Kwa mfano, mwalimu wa lugha anayetambua kwamba lugha ya Kiswahili ni muhimu kwa mtu aliyeimudu sawasawa katika soko la ajira;

- i. Ana imani kuwa lugha hiyo ni muhimu kufundishwa katika mfumo wa elimu wa nchi yake; (kiwango cha ufahamu)
- ii. Anafurahia vipindi vyake wakati anapoifundisha; (kiwango cha hisia)
- iii. Anaizungumza kwa ufasaha mara nyingi ili kuwatia motisha wanafunzi wake (vitendo).

Kwa hivyo, muundo wa mielekeo unabainisha uhusiano bayana baina ya vichocheo, mielekeo na mwitikio kutokana na utatu wa mielekeo. Uhusiano huo umewasilishwa katika kielelezo kifuatacho.

Mchoro: Uhusiano baina ya vichocheo, mielekeo na mwitikio kutokana na utatu wa mielekeo



Chanzo: Rosenberg na Hovland (1960) katika Bouzidi (1989)

Ijapokuwa mielekeo haidhihiriki waziwazi kwa kuichunza, ipo. Mielekeo huathiri na kuelekeza mwenendo wa matendo na tabia zinazoweza kudhihirika

waziwazi. Mielekeo inaweza kutambulika ama kupitia tabia zinazodhihirishwa na mtu, au kupitia mwitikio wake (unaodhihirisha tathmini hasi au chanya kuhusu kilengwa cha mielekeo) na hali ambamo tabia husika zinadhihirishwa (Ajzen, 1984). Kwa kiasi fulani, matendo na tabia ya mtu inaweza kutabirika kupitia kwa imani yake. Ndiposa Fishbein (1965) anaeleza kwamba tathmini za kuaminika kuhusu mielekeo zinaweza kupatikana wakati kauli au hoja mbalimbali kuhusu imani zinachunguzwa kwa pamoja. Katika utafiti huu, kauli kuhusu imani ya watafitiwa juu ya lugha ya Kiswahili zilishirikishwa ili kusaidia kubainisha mielekeo iliyoishikiliwa na walimu kuhusu Kiswahili.

Kuhusu njia na mbinu za kutafiti mielekeo, wataalamu wamekubaliana kwamba haitoshi kuchunguza tabia za mtafitiwa kuhusiana na kilengwa fulani (Fishbein, 1967 na Osgood, 1975). Hali za kiakili za watafitiwa zinapaswa kuchunguzwa pia (Agheyisi na Fishman, 1970). Wasomi wanaoegemea mkabala huu wanasisitiza kwamba ufahamu, hisia na matendo kuhusu kilengwa yanaweza kuathiri mielekeo kuhusu kilengwa na kwamba mielekeo hiyo pia inaweza kuathiri ufahamu, hisia na tabia ama matendo.

Binadamu hazaliwi na mielekeo, bali hujifunza kutokana na mambo na hali anazokumbana nazo (Mohochi, 2007). Utafiti umeonesha kwamba mielekeo ya watu hujengwa kutokana na mitagusano ya kifamilia katika asasi za kijamii ambapo watoto hujifunza kwa kuwaiga wazazi wao. Aidha, taasisi kama shule, sehemu za maabadi, vyombo vya habari na tajriba huchangia sana ujenzi wa mielekeo (Lambert na Lambert, 1964; Parsons *na wenzake*, 1982; Bouzidi, 1989; Garrett, 2010; Saldana, 2013; Strasburger na Wenzake, 2010; Moeller na Vreese, 2013; Philo na Happer, 2013). Kwa ujumla, anavyoeleza Mohochi (2007), binadamu hujenga mielekeo chanya kwa chombo ambacho kinampa manufaa fulani na mielekeo hasi kwa kile kisichoonesha manufaa yoyote kwake.

Lugha katika Jamii

Lugha ina majukumu muhimu ya kijamii. Ni chombo cha kupashana habari, kuanzisha na kudumisha mahusiano baina ya watu (Trudgill, 1992). Dirven (1994) ametaja dhima tatu za msingi ambazo kila lugha hutekeleza. Dhima hizi ni, uratibishaji wa kifahamu, mawasiliano na uratibu wa matabaka ya kijamii. Dhima ya uratibishaji wa kifahamu inahusiana na utambuzi kwamba lugha ni chombo ambacho binadamu huwasilishia ufahamu, mawazo na hisia zake. Ni chombo kinachotumiwa kufasili na kueleza uhalisia na tajriba za wanadamu mbali na kupanga mitizamo katika utamaduni kwa njia mahsusi (Dirven, 1994). Dhima ya pili ya lugha inahusiana na jinsi lugha inavyotumiwa kama chombo cha kimtagusano na mawasiliano. Ni sifa inayofungamanisha matukio uneni yote katika jamii. Dhima hii ndiyo inayoonesha kwamba lugha inasaidia kutambulisha na kuhifadhi watu binafsi na makundi ya kijamii (Wardhaugh, 1993).

Anavyosema Edwards (2009), dhana ya utambulisho inarejelea mfanano wa mtu kila wakati katika hali zote. Ni mwendelezo na hali ambapo kuna uzi unaosuka maisha mtu. Hali hii inamaanisha kuwa kuna muungano dhahiri kati ya utambulisho wa mtu binafsi na ule wa kikundi cha watu. Kwa kiwango cha mtu binafsi, utambulisho unampa mtu hakikisho la ukamilifu. Katika kiwango cha kikundi, muungano huo una asili yake katika historia na unaendelezwa kupitia utamaduni. Kwa hivyo, upekee wa mtu unatokana na uhusika wa sifa maalumu zinazochotwa katika bohari moja kuu kupitia mchakato wa utangamano wa kijamii. Basi lugha ni kitambulisho, siyo tu kwa kiwango cha mtu binafsi, bali pia kwa kundi nzima. Kwa ngazi ya mtu binafsi, kila mnenaji ana upekee wake wa matamshi na utumiaji lugha, ingawa mtu huyo huwa sehemu ya kundi nzima la watumiaji wa mfumo mahsusi.

Dhima ya lugha kama nembo ya kikundi ni bayana zaidi. Kila mtu huwa ameizoea lafudhi, lahaja na aina za lugha ambazo zinatambulisha ushirika wake katika jamii lugha mahsusi, tabaka la kijamii, makabila ya watu na makundi ya kitaifa. Kutokana na dhima hii, kwa mfano, tunapata wanenaji wa lugha tofauti kama vile Kibukusu, Kiekegusii, Kiluo na kadhalika. Kwa wazungumzaji wa Kingereza kwa mfano, kutokana na matumizi bainifu, kuna wazungumzaji wa tabaka la chini, wa tabaka la kati na wale wa tabaka la juu. Kwa mantiki hii kikundi kimoja kinaweza kutofautishwa na kikundi kingine cha watu kupitia kwa lugha inayotumiwa na washiriki wa makundi tofauti katika lugha moja na baina ya lugha zinazotumiwa baina ya makundi hayo (Coupland, 2007).

Dhima ya tatu ya lugha inarejelea dhana kwamba lugha inadhihirisha sifa za muundo na ruwaza za jamii. Hususan, mpangilio wa makundi katika jamii kimfumo, kuanzia kundi la chini hadi la juu hutegemea lugha. Webb na Kembo (2000) wakirejelea dhima hizi iwanasema kwamba majukumu ya lugha ni ya kimatumizi na kiishara. Kwao, dhima ya kimatumizi inarejelea lugha kama chombo cha kutekelezea jambo. Lugha inatumika kupasha habari, hisia na matamano ambayo ni muhimu katika mahusiano kati ya watu. Kwa muktadha wa dhima kimatumizi, lugha ni chombo cha kuwashirikisha watu katika matukio muhimu ya kijamii na kunufaika kutokana na ushiriki wao. Nchini Kenya, lugha ya Kingereza kwa muda mrefu imekidhi dhima ya lugha rasmi katika hali nyingi kama vile bungeni, kotini, diplomasia na biashara za kimataifa na kutumika shuleni kama lugha ya kufundishia. Kwa hivyo, wananchi wanaokosa ufahamu na ufasaha katika lugha hiyo wanakosa nafasi ya kushiriki katika maswala haya muhimu, na hivyo kukosa kupata manufaa yanayotokana nayo.

Webb na Kembo (2000) wanaeleza kwamba lugha pia ina dhima bainifu na tambuzi ambapo inatekeleza wajibu wa kutenga watu au makundi mbali na kuyatambulisha makundi ya watu kijamii. Dhima ya kiishara inayofafanuliwa inasawiana na maelezo ya Dirvan (1994), kwamba lugha hutumika kufasili na

kueleza uhalisia na tajriba za wanadamu mbali na kupanga mitizamo katika utamaduni kwa njia mahsusi.

Dhima hizi zinaashiria uhusiano uliopo kati ya lugha na jamii. Kwa kuwa lugha ni tukio la kijamii, imefungamana kwa karibu na miundo na maadili ya jamii ambapo lugha mbalimbali hutathminiwa kwa njia tofauti (Trudgill, 1992). Hali hii inasababisha ujenzi wa mielekeo kuhusu lugha tofauti. Mielekeo kubalifu inaelekezwa kwa lugha zinazotathminiwa kuwa za hadhi ya juu au zinazowapa watumiaji wake manufaa zaidi. Na mielekeo isiyo kubalifu inaelekezwa kwa lugha zinazoonekana kuwa za hadhi ya chini, ambazo zinachukuliwa kuwa hazina manufaa makubwa. Licha ya haya, mielekeo chanya inaweza kuundwa kwa lugha zenye hadhi ndogo kutokana na dhima yake ya kiushirika. Kwa mfano lugha ya Kiswahili nchini Kenya, ambapo ingawa imechukuliwa kuwa ya hadhi ya chini ikilinganishwa na Kingereza, imeibua mielekeo chanya kutokana na uwezo wake wa kuwaunganisha wananchi.

Mielekeo Lugha

Licha ya umuhimu wake kwa ukuaji na maendeleo ya lugha katika jamii, sera na upangaji wa lugha, mielekeo ya lugha ni eneo ambalo bado halijachunguzwa sana (Smit, 1996; Dirven, 1991; Baker, 1992). Mielekeo ya lugha kwa mujibu wa Ryan na wenzake (1982) ni misimamo ya kitathmini, kifahamu au kitabia inayoelekezwa kwa aina mbalimbali za lugha na wazungumzaji wake. Maelezo haya yanapanua vilengwa vya mielekeo ya lugha, ambapo siyo lugha tu inayoweza kuibua mielekeo, bali wazungumzaji wa lugha husika pia. Adegbija (2000) anaifafanua mielekeo ya lugha katika muktadha mpana unaojumuishia ukadiriaji wa tathmini kuhusu lugha, wazungumzaji wa lugha, juhudi za kuiendeleza lugha, kuihifadhi lugha mbali na kuwepo kwa mpango kuhusu lugha na ujifunzaji wa lugha husika. Mielekeo inapata umuhimu katika sera na upangaji wa lugha, elimu ya lugha, mikakati ya kuziendeleza lugha zilizo katika hatari ya kuangamia, makundi mbalimbali ya watumiaji wa lugha katika jamii na dhima za lugha husika katika jamii.

Fasili ya mielekeo ya lugha inayoshirikisha lugha na wazungumzaji wake ni mwafaka zaidi kwani kuna uhusiano wa karibu kati ya lugha na utambulisho wa jamii. Watu hujitambulisha kama washiriki wa kundi la kijamii kutokana na sifa mahsusi zinazowatambulisha. Asemavyo Hogg (1995) katika Kircher (2010) sifa hizo ni lugha, umri na jinsia. Tafiti nyingi zimebainisha kwamba lugha ni ishara na nembo muhimu ya jamii (Harmers na Blanc, 2000; Garrett na wenzake, 2003; Poll, 2005)

Ingawa mielekeo ya lugha ni tukio la kijamii, si lazima washiriki wa kundi la jamii husika wadhihirishe mielekeo inayofanana kuhusu lugha lengwa (Kircher, 2010). Kuna vigezo mbalimbali vinavyoathiri mielekeo ya watu binafsi, vikiwemo umri, jinsia, uwezo, usuli wa kiutamaduni na kiisimu (Baker, 1992).

Aidha elimu ya mhusika ina athari kubwa juu ya mielekeo yake (Beattie, 1982 katika Kircher, 2010). Athari na umuhimu wa vigezo hivyo, ndizo sababu zinazowafanya wana jamii-lugha moja kudhihirisha tofauti za kimielekeo kuhusu lugha.

Kuhusu athari hasi ya mielekeo ya lugha, Crystal (2000) anaeleza kuwa ukosefu wa mielekeo chanya kwa lugha inaididimiza lugha husika. Kwa hivyo, anapendekeza ukuzaji wa mielekeo chanya kuhusu lugha kama mkakati mojawapo wa kuhifadhi lugha. Pendekezo hili ni muhimu katika muktadha wa utafiti huu. Tunaamini kwamba maendeleo ya Kiswahili yatategemea kwa kiasi kikubwa mabadiliko ya kimielekeo. Vigezo vingine vinavyoathiri mielekeo ya lugha katika kiwango cha jamii ni hadhi na mshikamano. Lugha ina hadhi endapo inapohusishwa na mamlaka, uwezo wa kiuchumi na nafasi za kujiendeleza kitaaluma (Escheverria, 2005). Lugha inayosheheni sifa hizi inapewa hadhi kubwa na dhahiri. Sifa hizi mbili zinachangia sana katika ujenzi wa *mielekeo ya kimatumizi* na *mielekeo ya kiushirika*. Mtu hujenga mielekeo ya kimatumizi kutokana na manufaa anayopokea kihadhi na kikazi kwa sababu ya matumizi yake ya lugha husika. Kwa upande mwingine, lugha inayotathminiwa kwa kigezo cha mshikamano inaibua hisia za umoja, kuwavutia wanakikundi na kuwapa hisia ya ushirikiano (Ryan 1982 katika Kircher 2010). Kutokana na sifa hii, kuna ujenzi wa *mielekeo ya kiushirika* baina ya wanakikundi au wanajamii. Mahusiano haya yanajitokeza nchini Kenya kuhusu Kiswahili.

Baadhi ya tafiti zilizofanywa awali nchini Kenya zimeonesha kuwa lugha ya Kingereza inaenziwa kwa kuwa ndiyo lugha ya watu kujiendeleza kitaaluma na kiuchumi mbali na kuwapa uwezo wa kuwasiliana katika ngazi ya kimataifa. Lugha ya Kiswahili nayo inatekeleza dhima ya kuwaleta wananchi wa matabaka mbalimbali pamoja, kuondoa hisia za ukabila na kuendeleza umoja katika nchi (Mwangi, 1998; Kembo-Sure, 2001; Wamalwa na wenzie, 2013).

Mielekeo ya lugha ni muhimu kwa ukuzaji wa lugha. Hili ni eneo muhimu linalohitaji utafiti wakati wote kwa sababu ya athari za mielekeo katika maamuzi mbalimbali yanayohusiana na lugha katika jamii Mohochi (2005). Umuhimu wa mielekeo unajitokeza katika sera na upangaji wa lugha (Ageyisi na Fishman, 1970; Edwards, 1985; Giles na Robinson, 1990; Holmes, 1992; Baker, 1992; O'Rourke, 2005; Kircher, 2010). Kama walivyoeleza Baker (1992) na Aziakpono (2007) bila kuzingatia mielekeo ya lugha, huenda sera nzuri pamoja na kuwepo kwa fedha kusifanikishe utekelezaji wa sera hizo. Kwa hivyo, kufaulu au kutofaulu kwa maamuzi kuhusu lugha kunategemea mielekeo ya waliolengwa.

Katika muktadha wa kielimu nchini Kenya, lugha ya Kiswahili imefundishwa kama somo la lazima tangu kuanzishwa kwa mfumo wa elimu wa 8-4-4. Aidha limetahiniwa kwa kiwango cha mitihani ya kitaifa katika kipindi chote hicho cha mfumo huo wa elimu. Ilivyotarajiwa, hatua ya kulifanya kuwa somo la lazima

imesaidia sana kuikuza na kuiendeleza lugha hiyo katika maeneo mengi nchini. Licha ya maendeleo yaliyoshuhudiwa, kuna madai kupitia tafiti kadha yanayoashiria kwamba katika baadhi ya maeneo nchini, kuna mielekeo hasi kuhusu Kiswahili (Maloba, 2010; Owala, 2014). Mojawapo ya maeneo yaliyotajwa ni eneo la Nyanza.

Mielekeo Lugha ya Walimu kuhusu Kiswahili

Azma kuu ya utafiti huu ilikuwa kuchunguza mielekeo ya lugha ya walimu wa Kiswahili na wanafunzi wa shule za msingi kuhusu Kiswahili na jinsi mielekeo hiyo ilivyoathiri ujifunzaji wa Kiswahili. Makala haya yanawasilisha matokeo ya mojawapo ya malengo mahsusi yaliyoazimia kutambua mielekeo ya lugha ya walimu wa Kiswahili na ruwaza zao za matumizi ya lugha katika shule za msingi za Kaunti ya Siaya. Tulifanya hivyo tukizingatia kwamba tafiti kadha zilizofanywa katika eneo hilo zilishughulikia tu wanafunzi wa shule za upili. Kuna madai kwamba wakazi wa eneo la Siaya wana mielekeo hasi kuhusu lugha ya Kiswahili. Kijiografia, eneo hili linapatikana katika sehemu ya Nyanza, magharibi mwa Kenya. Wasailiwa waliteuliwa kutoka katika kaunti ndogo sita za Kaunti ya Siaya ambazo ni Siaya, Uguja, Ugenya, Gem, Rarieda na Bondo. Jumla ya walimu 34 kutoka katika shule za msingi 18 walishiriki katika utafiti.

Hojaji ya maswali kwa walimu ilitumiwa kupata data iliyochanganuliwa. Hajaji hiyo ilikuwa na kauli 24. Kila kauli ilikuwa na viteuzi vitano vya majibu. Kwa kila kauli chanya, kila kiteuzi kilipewa msimbo wa kitakwimu ifuatavyo: nakubali kabisa (5), nakubali (4), sina uhakika (3), nakataa (2) na nakataa kabisa (1). Utaratibu huu uligeuzwa ulipotumika kwa kauli zilizokuwa hasi. Kwa kauli hasi, majibu yalisimbwa ifuatavyo: nakubali kabisa (1), nakubali (2), sina uhakika (3), nakataa (4) na nakataa kabisa (5). Kauli ziligusia maeneo matatu ya mielekeo: hisia, ufahamu na tabia kwa kuzingatia Kiswahili katika elimu, Kiswahili na vyombo vya habari, Kiswahili na kanda ya Afrika Mashariki na Kati, Kiswahili na maendeleo ya kiuchumi na Kiswahili na umoja wa kitaifa. Pia ruwaza za matumizi ya lugha zilichunguzwa.

Majibu ya yalisimbwa na kuingizwa kwenye tarakilishi na yakachanganuliwa kihhibati kwa kutumia programu ya uchanganuzi wa data za sayansi-jamii. Vipimo vya kitakwimu vilivyotumika ni: kipimo cha T, uchanganuzi wa mwachano (Uchamwa) na uhusiano wa vigeu.

Matokeo: Alama za Mielekeo ya Walimu

Kulingana na mfumo uliotumika katika utafiti, alama zilikokotolewa kwa ngazi ya 1 hadi 5. Alama wastani 1.0 hadi 2.60 ziliashiria mielekeo hasi. Alama wastani 2.61 hadi 3.40 zikaashiria hali ya kutokuwa na uhakika. Na alama wastani 3.41 hadi 5.0 ziliashiria mielekeo chanya. Muhtasari wa matokeo ya mielekeo ya walimu yamewasilishwa katika jedwali lifuatalo.

Jedwali 1: Alama wastani za mielekeo ya Walimu

	Kipimo cha T						Maoni
	Wastani	Mchepuko	Kipimo	t	df	Thamani ya p	
Mielekeo ya Walimu	4.308	0.305	3.41	17.3 59	33	0.000 < 0.05	Mielekeo Chanya

Muhtasari wa alama wastani za mielekeo ya walimu, unaonesha kwamba:

- i. Alama wastani ya mielekeo ya walimu ni 4.0308, (alama mchepuko ikiwa 0.305) kwa kuzingatia kiwango cha uaminifu cha alama 0.05 (asilimia 95% ya uaminifu wa majibu).
- ii. Alama wastani ya mielekeo ni zaidi ya alama ya kipimo cha mielekeo ambayo ni 3.41.
- iii. Walimu wa Kiswahili katika shule za msingi za Kaunti ya Siaya wana mielekeo chanya kuhusu lugha ya Kiswahili.

Uchunguzi ulifanywa kuhusu sifa za walimu (jinsia, kiwango cha elimu, makazi na tajriba ya ualimu) ili kubaini athari yazo kwa uthabiti wa mielekeo ya walimu kuhusu lugha ya Kiswahili. Kipimo cha utabiri wa uwiano-vigeu kimstari, *linear regression*, kati ya vigeu kilichunguzwa. Uchanganuzi ulizingatia uwiano baina ya vigeu huru na vigeu tegemezi. Sifa za jinsia, kiwango cha elimu, makazi ya walimu na tajriba yao zilichunguzwa kama vigeu huru. Mielekeo ya lugha ya walimu ilichunguzwa kama kigeu kinachobadilika. Vigeu hivyo vilichunguzwa ili kuamua kama viliathiri mielekeo ya walimu kuhusu Kiswahili. Matokeo hayo yalilinganishwa na matokeo ya uchanganuzi wa mwanachano, *Uchamwa*, baina ya vigeu hivyo.

Matokeo ya uchanganuzi yalidhihirisha kwamba kati ya vigeu huru vilivyotajwa: jinsia, makazi, kiwango cha elimu na tajriba ya ufundishaji hakuna kimoja kilichokuwa na athari muhimu kwa mielekeo ya walimu wa Kiswahili katika Kaunti ya Siaya. Kigeu cha jinsia hakikuwa na athari muhimu kwa mielekeo kwa mujibu wa takwimu isomuhimu ya $[F(1,32)= 2.07, \text{thamani ya } p\text{-ikiwa } 0.160]$. Kigeu cha jinsia kilisababisha mwachano wa asilimia 1.6% kwa mielekeo, $R^2 = 0.016$. Matokeo ya kipimo cha beta isiyosanifu, $\beta=0.517, t=1.439, p\text{-} =0.160$ yanaonesha kwamba mielekeo ya walimu wa kiume haikuwa na tofauti muhimu na mielekeo ya walimu wa kike. Aidha, makazi ya walimu haikuathiri mielekeo yao kuhusu lugha ya Kiswahili kwa mujibu wa kipimo cha takwimu isomuhimu ya $[F(1,23)=1.52, p\text{-} =0.24]$. Makazi yalidhihirisha mwachano wa asilimia 11.7% baina ya mielekeo ya walimu kama ilivyowasilishwa na kipimo $R^2 = 0.0117$. Matokeo ya kipimo cha beta isiyosanifu, kwa makazi ya “mjini” ni $\beta=0.854, t=1.445, p\text{-} =0.162$ na ya “kitongoji cha mji” $\beta= -0.04, t=-0.082, p\text{-}$

=0.935, yanaonesha kwamba walimu wanaoishi mijini na wale wanaoishi katika vitongoji vya miji hawatofautiani kimielekeo na wale wanaoishi mashambani.

Uchunguzi huu ulitambua kwamba kiwango cha elimu ya walimu wa Kiswahili hakikuathiri mielekeo yao kuhusu Kiswahili. Mielekeo ya walimu wa kiwango cha vyeti vya ualimu na stahahada ilipolinganishwa na ile ya walimu wa kiwango cha digrii, matokeo yalionesha mwachano wa mielekeo kwa asilimia 7.3% kwa mujibu wa takwimu isomuhimu ya $[F(2,31)= 1.22, \text{thamani ya } p\text{- ikiwa } 0.309, \text{ na } R^2 = 0.073]$. Matokeo ya kipimo cha beta isiyosanifu kwa walimu wa stahahada yalikuwa $\beta=0.502, t= -1.03, p= 0.311$ na matokeo ya walimu wa digrii, yakawa $\beta= -0.596, t= -1.414, p= 0.167$. Matokeo haya yalionesha kwamba mielekeo ya walimu wa stahahada na wale wa digrii haikuwa na tofauti muhimu na mielekeo ya walimu wa vyeti vya ualimu katika Kaunti ya Siaya. Kwa hivyo, kiwango cha elimu ya walimu hakikuwa kigezo muhimu cha kutofautisha mielekeo yao.

Athari ya tajriba ya walimu kwa mielekeo pia ilichunguzwa. Matokeo yalionesha kwamba tajriba za walimu zilitofautiana. Baadhi ya walimu walikuwa na tajriba ya mwaka mmoja tu. Wengine, zaidi ya miaka kumi. Uchanganuzi wa mwachano wa mielekeo kwa kipengele hiki ulionesha kutokuwepo kwa tofauti muhimu kati ya walimu waliokuwa na tajriba ndogo sana ya kufundisha na wale waliokuwa tajriba ya zaidi ya miaka kumi kwa mujibu wa ukokotozi wa takwimu isomuhimu ya $F(2,251)= 721, \text{ thamani ya } p\text{- ikiwa } 0.548$.

Tajriba ilisababisha mwachano wa asilimia 6.9% kwa mielekeo ya walimu kwa kuzingatia kipimo cha $R^2 = 0.069$. Matokeo ya kipimo cha beta isiyosanifu kwa walimu wa tajriba ya mwaka 1 hadi miaka 5 yalikuwa , $\beta=0.115, t= 0.200, p= 0.843$. Matokeo ya walimu wa tajriba ya miaka 6 hadi miaka 10 yalikuwa, $\beta= 0.612, t= 1.026, p= 0.313$ huku tajriba ya walimu waliofundisha kwa zaidi ya miaka 10 ikiwa $\beta= -0.091, t= -0.149, p= 0.883$. Takwimu hizi zinaonesha kwamba mielekeo ya walimu waliokuwa kuwa na tajriba ndogo haikuachana kwa kiwango muhimu na walimu waliokuwa na tajriba kubwa.

Matokeo ya utafiti kuhusu viwango vya uhusiano na mwachano baina ya vigeu na mielekeo umeonesha kwamba vigeu havikuathiri kwa kiwango muhimu mielekeo ya lugha ya walimu. Mintarafu ya haya, baadhi ya wanaisimu (Edwards, 1984; Baker, 1992 na Mwangi, 1998) walieleza kwamba sifa za jinsia, umri na ushirika katika kikundi huchangia tofauti za mielekeo ya wahusika. Hata hivyo, tofauti muhimu kati ya sifa hizo hazikudhihirika katika utafiti huu. Mielekeo ya watafitiawa ilibainika kuwa thabiti.

Aidha, athari ya jinsia na kiwango cha elimu kwa mielekeo ilichunguzwa. Matokeo yalionesha kwamba hapakuwepo na tofauti muhimu baina ya mielekeo ya walimu wa kike na wa kiume. Pia, matokeo yalionesha kwamba hakuna athari muhimu ya kigezo cha kiwango cha elimu cha walimu kwa mielekeo yao.

Walimu waliokuwa na cheti cha ualimu, wale wa stashahada na waenzao wa cheti cha digrii walibainisha mielekeo chanya. Ingawa imetajwa kwamba mielekeo huathiriwa na kiwango cha elimu ya mhusika (Beattie, 1982 katika Kircher, 2010), matokeo ya utafiti huu kuhusu mielekeo ya walimu hayakuunga mkono madai hayo. Wataalamu hao waliwachunguza watoto wa miaka kati ya 9 hadi 17. Imetajwa kwamba watoto katika kiwango hiki hukosa uthabiti kimielekeo kwa kuwa wangali katika kipindi cha ukuaji (Khasinah, 2014). Hata hivyo katika utafiti huu, watafitiwa wote walikuwa watu wazima ambao huenda mielekeo yao ya lugha ilikuwa imefikia kiwango cha uthabiti.

Mwitikio wa Walimu kwa Baadhi ya Kauli za Mielekeo

Tulichunguza majibu ya walimu kwa baadhi ya kauli walizopewa ili tubaini yalivyochangia alama wastani ya mielekeo. Kauli hizo ziliangazia hali ya Kiswahili katika elimu, maendeleo ya kiuchumi, vyombo vya habari miongoni mwa maeneo mengine. Mwitikio mahsusi wa walimu ulituchorea picha halisi kuhusu maoni na msimamo wao kuhusu lugha ya Kiswahili.

Elimu ya lugha ni sehemu ya mtaala wa masomo ya shule za msingi nchini Kenya. Walimu waulizwa iwapo *ufundishaji wa Kiswahili katika shule za msingi una manufaa kwa wanafunzi*. Kauli hii ilikuwa chanya. Asilimia 100% ya walimu walikubaliana nayo. Alama wastani ya majibu yao ilikuwa 4.65, alama mchepuko ikiwa 0.485. Ili kupima uthabiti wa majibu yao, walipewa hoja hasi iliyosema kwamba *kufundisha Kiswahili shuleni ni sawa na kupoteza wakati*. Asilimia 97% ya watafitiwa walipinga kauli hiyo na asilimia 3% wakikubali. Alama wastani za kauli hii zilikuwa 4.88 na alama mchepuko 0.686. Ni bayana kuwa walimu wanaamini kuwa kufundisha Kiswahili kuna manufaa siyo kwao tu bali pia kwa wanafunzi.

Ufundishaji wa Kiswahili kama somo la lazima ni suala lililojadiliwa katika eneo la utafiti (Mwanga, 1998; Owala, 2014). Kutokana na matokeo duni katika mitihani ya kitaifa na hali kwamba Kiswahili ni lugha ya Kibantu, wengi wa wakazi wa Nyanza wamekiri kuwa na ugumu wa kujifunza Kiswahili. Kwa hivyo, watafitiwa walipewa kauli kwamba *Kiswahili kisifundishwe shuleni kama somo la lazima*. Asilimia 85% waliipinga kumaanisha kuwa walikuwa na msimamo chanya kuhusu kauli hiyo. Walioonesha msimamo hasi walikuwa asilimia 15%. Alama za wastani kwa kauli hii zilikuwa 4.27, alama ya mchepuko ikiwa 1.442. Kutokana na majibu hayo, tulibaini nia ya baadaye ya walimu kuhusu Kiswahili. Waliombwa kuonesha msimamo wao kwa kauli kuwa *nikipewa nafasi ya kujiendeleza kimasomo nitasoma somo la Kiswahili*. Kauli hii ililenga kutambua nia ya utendaji wa watafitiwa katika siku za usoni. Kati ya wasailiwa 34, asilimia 94% walionesha msimamo wa kuteua somo la Kiswahili. Ni asilimia 6% pekee walioonesha msimamo hasi. Ikizingatiwa kwamba alama

wastani kwa kauli hii ilikuwa 4.64 na alama mchepuko ikiwa 0.603, huu ulikuwa msimamo wa kiwango cha juu cha uchanya.

Nchini Kenya, Kingereza ndiyo lugha ya kufundishia katika mfumo wa elimu. Kwa hivyo, kuna mitazamo kwamba imepewa hadhi ya juu kuliko Kiswahili (Owala, 2014). Kutokana na maoni haya, walimu walipewa kauli iliyosema, *walimu wa Kiswahili hawapewi heshima kama walimu wa masomo mengine*. Ikizingatiwa kwamba kauli hii ni hasi, asilimia 64% walikataa, ikiashiria kwamba kwa hakika walimu wa Kiswahili hupewa heshima. Ni asilimia 24% waliokubali kuwa walimu wa Kiswahili hawaheshimiwi huku asilimia 12% wakiwa na msimamo wa kadri. Alama wastani kwa matokeo ya kauli hii ni 3.59 nayo alama mchepuko ni 1.282. Ni jambo linaloashiria mustakabali mzuri wa Kiswahili kwani hii ni dalili kwamba hadhi yake inapanda huko mashinani.

Mbali na kuchunguza hadhi waliyopewa walimu wa Kiswahili wakilinganishwa na walimu wa masomo mengine, maoni ya walimu yalichunguzwa iwapo walihisi upungufu wowote kitaaluma kwa kusoma Kiswahili. Walijibu kauli iliyosema; *nikiwa mwalimu wa Kiswahili, nahisi kwamba sijaelimika sana*. Asilimia 82% ya walimu hawakuafikiana na kauli hii. Asilimia 15% (ikiwa ni walimu 5) ndio waliokuwa na maoni kwamba walijihisi kutoelimika sana kwa kusoma Kiswahili. Alama wastani kwa kauli hii aidha ilikuwa juu, yaani 4.15, kumaanisha kuwa walimu walikuwa na mwelekeo chanya. Hili huenda lilichangiwa na hali kwamba wataalamu wengi wa Kiswahili hivi sasa wametambuliwa na kuteuliwa katika nyadhifa za juu serikalini na katika mashirika ya serikali. Hata hivyo, suala la ufundishaji lilibainisha tofauti katika ruwaza za majibu ya walimu. Ufundishaji wa Kiswahili katika shule za msingi unazingatia vipengele vya sarufi na uandishi wa insha. Kwa hivyo, maoni ya walimu kuhusu uwezo wao wa kufundisha Kiswahili yalichunguzwa kupitia kauli kwamba *kufundisha sarufi na insha ya Kiswahili hakunipi matatizo*. Majibu kwa kauli hii yalikuwa kwamba asilimia 59% walikubali kwamba hawakupata matatizo katika ufundishaji wao. Nao asilimia 35% walidai kupata matatizo katika ufundishaji wao. Waliokuwa na msimamo wa kadri walikuwa asilimia 6%. Matokeo haya yamewasilishwa katika jedwali lifuatalo.

Jedwali 2: Walimu wanaopata ugumu wanapofundisha Kiswahili

Viteuzi	Idadi tokezi	Asilimia	Alama Wastani
Nakubali	20	59	3.29
Sikubali	12	35	Alama mchepuko
Sina Uhakika	2	6	1.268
Jumla	34	100.0	

Alama wastani kwa kauli hiyo ilikuwa 3.29 na alama mchepuko ikawa 1.268. Kwa kuwa alama ya kipimo cha mielekeo chanya kilikuwa 3.41, ina maana

kwamba matokeo ya kauli hii yalikuwa chini ya kipimo hicho. Yanaashiria kuwa walimu hawakuwa na uhakika kama walipata ugumu wakifundisha vipengele muhimu katika mtaala wa Kiswahili shuleni. Matokeo haya yanaashiria hali ya Kiswahili kielimu katika eneo la Siaya.

Mwangi (1998) katika utafiti alioufanya katika tarafa ya Maseno alisema kwamba wanafunzi walikiri kuwa walipata matokeo mabaya kwa sababu ya kupata ugumu wa kuelewa baadhi ya vipengele walivyofundishwa. Ingawa utafiti huu haukuthibitisha dai hili kikamilifu, tulibaini kuwa asilimia 35% ya walimu walipata ugumu wakifundisha vipengele vya sarufi. Idadi ya walimu 12 waliokiri kupata matatizo si ndogo ikilinganishwa na walimu 20 waliokiri kutopata shida. Huenda hali hiyo iliathiri ujifunzaji lugha wa wanafuzi.

Katika shughuli za kielimu, lipo pendekezo kwamba lugha ya Kiswahili itumiwe katika shughuli ya ufundishaji (Chimera, 1998; Muthwii, 2002; Mohochi, 2005). Hata hivyo pendekezo hili limepingwa kwa sababu kwamba Kiswahili hakijakomaa kutekeleza wajibu huo. Kwa hivyo msimamo wa walimu ulibainishwa kuhusu mjadala huo kwani wao ndio watekelezaji wa mtaala. Kwa hivyo, waliulizwa maoni kuhusu hoja iliyosema *lugha ya Kiswahili ina uwezo wa kutumiwa kufundishia sayansi na hesabu*. Asilimia 63% walikubali kwamba Kiswahili kinaweza kutekeleza dhima ya kufundishia sayansi na hisabati. Ni asilimia 21% walioonesha kwamba Kiswahili hakina uwezo huo. Asilimia 15% hawakuwa na uhakika kuhusu uwezo wa Kiswahili kufundishia sayansi na hisabati. (Tazama jedwali 3).

Jedwali 3: Uwezo wa Kiswahili kufundishia sayansi na hesabati

Mwitikio	Idadi tokezi	Asilimia	Alama wastani
Chanya	21	63	3.48
Hasi	8	22	Alama mchepuko
Wasio na hakika	5	15	1.176

Mielekeo ilikuwa chanya kuhusu uwezo wa Kiswahili kufundishia sayansi. Ingawa kiwango cha ukubalifu (3.48) siyo kikubwa sana kikilinganishwa na alama ya kipimo cha mielekeo (3.41), ni hatua nzuri ya kufahamu maoni ya walimu kuhusu dhima ya lugha ya Kiswahili katika elimu. Huenda maamuzi haya yaliongozwa na hali kwamba sasa Kiswahili kimetanuka na kina istilahi za kitaaluma katika tiba, kemia, biashara na tehamu miongoni mwa masomo mengine. Aidha, nchini Tanzania, Kiswahili ndiyo lugha ya kufundishia katika kiwango cha shule za msingi. Kwa hivyo Kenya haitakuwa nchi ya kwanza kufanya jaribio hilo. Isitoshe, lugha ya Kiswahili inatumika kufundishia somo la Kiswahili hadi ngazi ya chuo kikuu. Ina maana kwamba ina uwezo wa kiakademia.

Mielekeo kuhusu nafasi ya lugha ya Kiswahili kama lugha ya ukanda wa Afrika Mashariki, kati na ulimwenguni kote, ilichunguzwa. Matokeo yamewasilishwa. Kauli: *lugha ya Kiswahili ina uwezo wa kuunganisha bara la Afrika.*

Jedwali 4: Uwezo wa Kiswahili kuunganisha bara la Afrika

Mwitikio	Idadi tokezi	Asilimia	Alama wastani
Chanya	31	91	4.45
Hasi	1	3	Alama mchepuko
Wasio na hakika	2	6	0.754

Asilimia 91% walibainisha mielekeo kubalifu kuhusu nafasi ya Kiswahili kuunganisha bara la Afrika. Ni idadi ndogo tu, asilimia 3% pekee iliyokuwa na maoni kinyume. Kauli iliyoendana na hii ililenga kutambua ufahamu wa walimu kuhusu eneo la Kiswahili linalozidi kupanuka. Walipewa kauli iliyosema, *umuhimu wa Kiswahili unazidi kuongezeka katika dunia ya leo.* Majibu ya walimu yamewasilishwa katika jedwali 6.

Jedwali 5: Umuhimu wa Kiswahili unazidi kuongezeka ulimwenguni

Mwitikio	Idadi tokezi	Asilimia Kubalifu	Alama wastani
Chanya	31	88	4.33
Hasi	1	3	Alama mchepuko
Wasio na hakika	2	9	0.89

Kuna utambuzi mkubwa (kwa asilimia 88%) kuhusu ongezeko la nafasi ya Kiswahili duniani. Ili kuthibitisha majibu yao, waliulizwa kuhusu haja ya wageni wanaozuru Kenya kujifunza lugha ya Kiswahili. Kauli ilisema, *wageni wote wanaozuru Kenya wanapaswa kujifunza Kiswahili.* Nia ya kauli hiyo ilikuwa kupata uelewa kuhusu umuhimu wa Kiswahili kimawasiliano na kupima iwapo misimamo yao ingebakia thabiti katika kuonesha kuwa Kiswahili ni lugha muhimu. Asilimia 73% walisema ni muhimu wageni wajifunze Kiswahili. Asilimia 18% hawakuona ulazima huo. Asilimi 9% ya walimu hawakuwa na hakika. Ni dhahiri kwamba Kiswahili ni lugha muhimu, siyo tu kama lugha ya mawasiliano, bali kama nyenzo ya kupasha utamaduni wa kifarika kwa wageni wanaozuru nchi ya Kenya.

Kisha, maoni kuhusu nafasi ya vyombo vya habari katika ukuzaji wa mielekeo chanya kuhusu Kiswahili yalichunguzwa. Vyombo vya habari, hasa redio vinategemea lugha kama nyenzo muhimu ya kutimiza wajibu wavyo. Kauli kuwa *redio za kienyeji zinapaswa kuwa na vipindi maalumu kwa lugha ya Kiswahili* ilijibiwa. Asilimia 97% ya watafitiwa walikuwa na mwitikio chanya

kuhusu kauli hiyo. Ni asilimia 3% pekee waliokuwa na mwitikio hasi. Alama wastani kwa kauli hii ni 4.58. Ni bayana kwamba walimu wanatambua nafasi inayotekelezwa na vyombo vya redio katika kukuza lugha ya Kiswahili.

Majibu kwa kauli za mielekeo yalithibitisha matokeo chanya ya kipimo cha T ya mielekeo ya walimu. Imebainika kwamba walimu wanaamini katika uwezo wa lugha ya Kiswahili. Mielekeo yao kwa Kiswahili ni ya kiushirika na kimatumizi. Wanaiona lugha ya Kiswahili siyo tu kama chombo cha kuleta utangamano katika jamii, bali pia kama chombo cha manufaa ya kiuchumi na kielimu.

Ruwaza za Matumizi Lugha ya Walimu

Mbali na kuchunguza mielekeo ya walimu kuhusu lugha ya Kiswahili, uchunguzi wa ruwaza za matumizi ya lugha ya walimu ulifanywa. Uchunguzi wa ruwaza za matumizi ya lugha ni muhimu kwa kuwa ndio msingi wa kufafanua hali ya lugha ilivyo kwa wakati uliopo. Ufafanuzi wa ruwaza pia ni msingi wa kufanya utabiri wa hali itakavyokuwa katika miaka ya baadaye (Msanjila, 2007). Shuleni, walimu ni mifano ya kuigwa na wanafunzi. Kwa hivyo, ujenzi wa mielekeo mipya inaathiriwa pakubwa na nafasi yao. Kama alivyosema Mohochi (2005), shule zinatoa mchango mkubwa katika kuikua mielekeo ya wanafunzi na kuifanya kuanza kutofautiana na ile ya wazazi wao. Kwa hivyo uchunguzi wa ruwaza za matumizi ya lugha ya walimu unaweza kutuanguzia athari yao kwa wanafunzi kutokana na jinsi wanavyotumia lugha wanapokuwa katika mazingira ya shuleni.

Ruwaza za matumizi ya lugha zilichunguzwa kwa kuzingatia mawanda muhimu ya matumizi. Ufafanuzi wa hali halisi ya matumizi ya lugha ya walimu katika eneo la utafiti ulifanywa. Matokeo yalikuwa msingi wa kuamua jinsi lugha zilivyotumika katika mawanda mbalimbali na kukadiria kama matumizi hayo yalikuwa na athari kwa mustakabali wa Kiswahili kwa ujumla. Swali lililoongoza ufasiri huo lilikuwa: Je, Kiswahili kilipewa nafasi ipi katika matumizi ya lugha ya walimu? Kwa kufanya hivyo, thamani iliyopewa lugha ya Kiswahili kama lugha ya mawasiliano katika shughuli za kila siku za walimu ilikadiriwa. Ruwaza za matumizi ya lugha ya walimu zilichunguzwa kwa mujibu wa mawanda ya matumizi ya lugha kufuatia misingi ya Nicolle (2019). Aliyafafanua mawanda ya matumizi ya lugha kuwa muungano wa nyakati bainifu, mandhari mahsusi na dhima za kimahusiano. Katika uchunguzi huu, mawanda yafuatayo yalijumuishwa: mawanda ya kifamilia, mawanda ya sikoni, mawanda ya kidini, mawanda ya kijamii, mawanda ya kielimu na mahali pa kazi.

Uchanganuzi wa matokeo ya ruwaza za matumizi ya lugha ulionyesha kwamba idadi kubwa ya watafitiwa, asilimia 68%, asilimia 50%, asilimia 44%, asilimia 68% na asilimia 44% walitumia mseto wa Kiswahili na Kingereza walipohutubu kwenye gwaride, walipokuwa ofisini na walimu wenzao,

walipowasiliana na wanafunzi wao shuleni na walipokuwa katika mikutano shuleni mwao mtawalio.

Ni asilimia 12% waliotumia Kiswahili pekee kwenye gwaride. Ofisini, asilimia 9% tu ya walimu walitumia Kiswahili kuwasiliana. Katika mawasiliano na walimu wenzao, asilimia 18% walitumia Kiswahili. Matumizi baina ya walimu na wazafunzi wao na baina ya walimu na wenzao yalifanana ambapo asilimia 18% ya walichagua kutumia Kiswahili. Katika mikutano rasmi shuleni, asilimia 9% tu walitumia Kiswahili pekee bila kuchanganya ndimi.

Matokeo haya yalionesha picha halisi kwamba katika mazingira yaliyo rasmi shuleni, mseto wa lugha ya Kingereza na Kiswahili ulitumika kwa wingi kuliko lugha ya Kiswahili pekee. Tulipolinganisha takwimu za alama wastani katika asilimia za matumizi ya lugha hizo, ilikuwa bayana kwamba kwa ujumla matumizi ya mseto wa Kingereza na Kiswahili ni asilimia 58.8% na alama wastani za matumizi ya Kiswahili pekee zikiwa 13.2%. Tofauti kati ya alama hizi ni 45.6. Tofauti hii ni kubwa na muhimu ikizingatiwa kwamba walimu walibainisha kuwa na mielekeo chanya kuhusu Kiswahili. Ulinganishi wa matumizi ya Kingereza dhidi ya Kiswahili katika mawanda haya ulionesha kuwa kwenye gwaride, ni asilimia 9% waliotumia Kingereza. Waliotumia Kiswahili kwenye gwaride ni asilimia 12%. Matumizi ya Kingereza yaliongezeka katika mawasiliano walipokuwa ofisini, yakiwa asilimia 21% huku yale ya Kiswahili yakipungua na kuwa asilimia 9%. Hata hivyo mawasiliano ya walimu na wenzao yaliakisi matumizi mengi ya Kiswahili, ikiwa ni asilimia 18%, na Kingereza kikitumiwa na asilimia 9%. Kwa ujumla, uchambuzi ulionesha kwamba idadi kubwa ya walimu walipenda kuchanganya msimbo hususan Kingereza na Kiswahili walipokuwa katika mazingira ya kazini.

Katika mawanda hayo, asilimia 12% ya watafitiwa walitumia mseto wa Kingereza, Kiswahili na Kijaluo kuhutubu kwenye gwaride. Matumizi ya mseto huo yaliongezeka ofisini, ambapo walioteua kutumia misimbo hiyo walikuwa asilimia 21%. Aidha, ruwaza hiyo ilitumika zaidi baina ya walimu na wenzao kwa asilimia 29%. Ni dhahiri kwamba, baada ya matumizi ya mseto wa Kingereza na Kiswahili, ruwaza inayofuata kwa kuwa na matumizi mengi miongoni mwa walimu ni mseto wa Kingereza, Kiswahili na Kijaluo.

Kuwepo kwa matumizi mengi ya Kiswahili, licha ya kujitokeza kwa mseto na Kingereza na Kijaluo kunaunga mkono matokeo kuhusu mielekeo ya walimu. Ingawa lugha ya Kijaluo (kama msimbo mmoja) haikutumika kwenye gwaride, asilimia 3% ya walimu walionesha kuitumia katika mawasiliano yao na wanafunzi shuleni. Huenda hali hiyo ilitokana na sababu kwamba walimu wa shule za msingi walipangiwa kazi kuanzia madarasa ya chini hadi ya juu. Mwalimu anapopangwa kufundisha darasa la awamu ya chini, hana budi kutumia

Kijaluo kwa kuwa wanafunzi wa awamu hiyo ndipo huwa wanatangulizwa kwa somo la Kiswahili, baadhi yao huwa hawajui lugha kabisa.

Mawasiliano baina ya walimu na wazazi yalidhihirisha tofauti kubwa katika uteuzi wa lugha. Asilimia 44% walitumia mseto wa Kingereza, Kiswahili na Kijaluo. Aidha, matumizi ya Kijaluo yalipata kuongezeka kwani asilimia 26% waliitumia kuwasiliana na wazazi. Mseto wa Kiswahili na Kingereza ulitumiwa na asilimia 12% sawa na Kiswahili pekee ambapo asilimia 12% ya walimu waliitumia. Lugha iliyotumiwa kwa uchache zaidi ilikuwa Kingereza ambapo asilimia 6% pekee ya walimu waliitumia. Matokeo haya yaliashiria kwamba ingawa walimu na wazazi waliwasiliana kwa kutumia Kiswahili, Kiluo na Kingereza, matumizi mengi yalichanganya ndimi na misimbo iliyohusisha Kiswahili.

Ruwaza za matumizi ya lugha zilibadilika sana matumizi yalipochunguzwa katika mawanda nje ya shule. Mawanda hayo yalikuwa: kanisani, sokoni na familia. Walipokuwa kanisani, asilimia 39% walitumia msimbo wa kuchanganya ndimi ambapo Kingereza, Kiswahili na Kijaluo zilitumika kwa mseto. Aidha, lugha ya Kijaluo ilipata matumizi mengi ambapo asilimia 27% walidai kuitumia. Mseto wa Kiswahili na Kingereza ulitumiwa na asilimia 18% huku Kiswahili pekee kikitumiwa na asilimia 15% ya walimu. Ilibainika kwamba katika matumizi ya lugha kanisani, hakukuwepo na matumizi ya lugha ya Kingereza peke yake.

Katika shughuli za kibiashara sikoni, lugha iliyotumika kwa asilimia kubwa ilikuwa Kijaluo, kwa asilimia 35%. Matumizi ya mseto wa Kingereza, Kiswahili na Kijaluo na matumizi ya Kiswahili yalikuwa asilimia 24% mtawalio. Kiswahili pekee kilikuwa na matumizi kwa asilimia 6%. Hata hivyo, katika mawanda ya sokoni, asilimia 12% walikiri kutumia lugha nyinginezo. Ikizingatiwa kuwa Kaunti ya Siaya ina ujirani na maeneo ya wazungumzaji wa lugha za nyingine za Kibantu, matokeo haya yalidhihirisha ukweli huo. Hata hivyo, katika mawanda ya sokoni, hakuna walimu waliotumia lugha ya Kingereza peke yake.

Matumizi ya lugha baina ya walimu na watu wa jamaa zao yalibainisha ruwaza tofauti na mawanda hayo mengine. Lugha iliyotumiwa zaidi, kwa asilimia 29% ilikuwa Kijaluo. Ilifuatwa na matumizi ya mseto wa Kingereza, Kiswahili na Kijaluo kwa asilimia 24%. Mawasiliano baina ya wanajamii pia yalidhihirisha matumizi ya lugha nyinginezo kwa asilimia 12%. Matumizi ya Kiswahili pekee yalikuwa asilimia 21% huku mseto wa Kingereza na Kiswahili ukitumika kwa asilimia 9% pekee. Lugha iliyotumiwa kwa nadra ilikuwa Kingereza kwa asilimia 6%.

Kutokana na uchanganuzi wa ruwaza za matumizi ya lugha ya walimu, tulifikia mahitimisho yafuatayo:

- i. Matumizi mengi ya lugha ya walimu yalikuwa ya kuchanganya misimbo, hususan Kingereza na Kiswahili walipowa katika mazingira ya shuleni.
- ii. Msimbo wa kuchanganya ndimi tatu: Kingereza, Kiswahili na Kijaluo ulipendelewa sana katika miktadha ya mawasiliano baina yao na wazazi, na kanisani.
- iii. Katika miktadha ya nje ya shule, lugha ya matumizi iliyopendelewa sana ilikuwa Kijaluo.
- iv. Ingawa matumizi ya lugha ya Kiswahili peke yake yalikuwa ya chini (tukilinganisha matumizi kwa asilimia), yalijitokeza katika mawanda yote. Hiyo ni ishara ya kukua kwa Kiswahili katika kaunti. Inaashiria kwamba lugha hiyo imepenya na inaendelea kukubalika katika mawanda mengi ya kijamii katika Kaunti ya Siaya.

Hitimisho

Makala haya yameonesha kwamba mielekeo ni sehemu ya maisha ya binadamu. Wanadamu huwa na mielekeo ama chanya au hasi kwa vilengwa mbalimbali kwa kutegemea tathmini wanazovifanyia vilengo hivyo. Pia makala yameonesha kwamba mielekeo kuhusu lugha hujengwa kwa kutegemea dhima hadhi zinazopewa lugha tofauti katika jamii. Matokeo ya utafiti kuhusu mielekeo ya walimu wa Kiswahili katika shule za msingi yameonesha kwamba walimu wanaofundisha Kiswahili katika shule za msingi walikuwa na mielekeo chanya kuhusu Kiswahili. Aidha, matumizi ya lugha ya walimu katika mawanda mbalimbali yalionesha kuwepo kwa matumizi ya Kiswahili. Ugunduzi huu ni muhimu kwa maendeleo ya Kiswahili. Kinyume na madai yaliyokuwepo kwamba wakazi wa eneo la nyanza walikuwa na mielekeo hasi kuhusu Kiswahili, matokeo haya yanadhihirisha kwamba hali zimezidi kubadilika. Mustakabali wa Kiswahili ni mzuri katika eneo la Siaya.

Marejeleo

- Adegbija, E. E. (2000). Language Attitudes in West Africa. *International Journal of the Sociology of Language*, 141, 75-100.
- Agheysi, R., & Fishman, M. (1970). Language Attitude Studies: A Brief Survey of Methodological Approaches. *Anthropological Linguistics*, 12(5), 137-157.
- Ajzen, I. (1989). *Attitudes, Personality and Behaviour*. Milton Keynes: Open University Press.
- Bohner, G. (2001). Attitudes. Kwenye H. A. Hewstone, *Introduction to Social Psychology*, 3rd Edition (kur. 239-282). Oxford: Basil Blackwell.
- Bouzidi, H. (1989). *Language Attitudes and Their Implications for Education: Morocco as a Case Study*. University of Glasgow: Unpublished PhD Thesis.

- Coupland, N. (2007). *Style, Language Variation and Identity*. New York: Cambridge University Press.
- Dirven, R. (1994). *Contact and Conflict Linguistics in Southern Africa*. Duisburg: L.A.U.D.
- Edwards, J. (2009). *Language and Identity: An Introduction*. New York: Cambridge University Press.
- Eiser, J., & Plight, J. (1988). *Attitudes and Decisions*. New York: Routledge.
- Escheverria, B. (2005). Language Attitudes in San Sebastian: The Basque Vernacular as Challenge to Spanish Language Hegemony. *Journal of Multilingual and Multicultural Development*, 26 (3) 249-264.
- Gardner, R. (1985). *Social Psychology and Second Language Learning: The Role of Attitudes and Motivation*. London: Edward Arnold.
- Garrett, P. (2010). *Attitudes to Language*. New York: Cambridge University Press.
- Garrett, P., Coupland, N., & Williams, A. (2003). *Investigating Language Attitudes: Social Meanings of Dialect, Ethnicity and Performance*. Cardiff: University of Wales Press.
- Kircher, R. (2010). *Language Attitudes in Quebec: A Contemporary Perspective*. University of London: PhD Thesis.
- Lambert, W. E., & Lambert, W. (1964). *Social Psychology*. New Jersey: Engelwood Cliffs.
- Maloba, M. (2010). The Influence of Students Attitudes Towards Learning Kiswahili on their Performance in Rachuonyo District: Strategies, Programmes and Clubs for Attitude Change. *International Conference on Bilingualism and Teaching*. Kenyatta University.
- Mohochi, E. S. (2005). *Mielekeo ya Wanafunzi Kuhusu Kiswahili na Athari zake Katika Matokeo ya Mtihani wa Kiswahili wa Kidato cha Nne katika Mikoja ya Pwani na Nyanza, Kenya*. Chuo Kikuu cha Egerton: Tasnifu ya Uzamifu.
- Mohochi, E. S. (2007). Mielekeo ya Wanafunzi Kuhusu Lugha ya Kiswahili na Athari Zake katika Matokeo ya Mtihani wa Kiswahili wa Kidato cha Nne katika Mikoja ya Pwani na Nyanza, Kenya. Katika F. Senkoro, *Lugha na Fasihi ya Kiswahili Afrika Mashariki*. Dar es Salaam: CHAKAMA.
- Mohochi, E. S. (2011). Mielekeo ya Wasomi wa Kiswahili na Viongozi wa Afrika Mashariki kuhusu Lugha ya Kiswahili. *Swahili Forum*, 18, 24-36.
- Msanjila, Y. (2007). Utumiaji wa Kiswahili na Lugha za Jamii Kijinsia Nchini Tanzania. *Nordic Journal of African Studies*, 16(1), 18-29.
- Mwangi, P. (1998). *Uhusiano Uliopo kati ya Mitazamo ya Lugha ya Wanafunzi wa Kidato cha Nne na Utendaji wao: Hali ya Kiswahili katika Tarafa ya Maseno*. Chuo Kikuu cha Moi: Tasnifu ya Uzamili.

- Nicolle, S. (2019). *Sociolinguistics: Multilingualism and Diglossia*. Imechukuliwa toka Academia.edu: <http://www.academia.edu>
- Osgood, C. (1957). *The Measurement of Meaning*. Urban: University of Illinois Press.
- Philo, G., & Happer, C. (2013). The Role of Media in the Construction of Public Belief and Social Change. *Journal of Social and Political Psychology*. Vol. 1 (1) pp 321-336.
- Saldana, J. (2013). Power and Conformity in Today's Schools . *International Journal of Humanities and Social Sciences*, Vol. 3(1), 228-232.
- Trudgill, P. (1992). *Introducing Language and Society*. Harmondsworth: Penguin Books.
- Wamalwa, E. W., Adika, S. K. & Kevogo, A. U. (2013). Multilingualism and Language Attitudes: Students Perceptions towards Kiswahili in Mtwara Region of Tanzania. *Research on Humanities and Social Sciences*, Vol. 3 No. 12, 53-65.
- Wardhaugh, R. (1993). *Investigating Language: Central Problems in Linguistics*. Oxford: Basil Blackwell.
- Webb, V., & Kembo-Sure. (2000). *African Voices: An Introduction to the Language and Linguistics of Africa*. Oxford: Oxford University Press.
- Zimbardo, P., & Leippe, M. (1991). *The Psychology of Attitude Change and Social Influence*. Philadelphia, PA: Temple University Press.

